

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
11 Julai 2009**

Waliohudhuria

Juma Ali Salehe Jongo
Mohammed Samwely
Omary Shabani
Abdul H Mwaibambe
Beda John Mkusu
Hamadi Hatibu Bwaja
Shamte J Kisoma
George Salustian Mgata
Shukuru Hassan
Kibwana Mohammad Msiga
Filbert Mbecha
Elaine Baker
Athumani Mussa Kitemo
Sosthenes C Amlima
Saidi Brashi
Bashiri Rashidi
Ally Salum
Juma Hassan Chibaya
George Kabogo
Rahma Ali
Paulo Atibu Hatibu
Mussa Omari
Ally Athuman Jumbe

Wageni

Bjorn Stafbom, mtalaamu wa usalama barabarani, Benki ya Dunia, Merikani
Adrian Walsh, mtalaamu wa usalama barabarani, Global Transport Knowledge
Partnership GTKP
Kate McMahon, mtalaamu wa usalama barabarani, Serikali ya UK

Ishaku Bamaiyi, Nigeria

Wageni

Wakati wa mkutano wageni waliohudhuria mkutano wa usalama barabarani wiki hii walitembelea ofisi yetu – kwanza Bjorn Stafbom, Adrian Walsh na Kate McMahon waliofika na baisikeli na baadaye Ishaku Bamaiyi aliyefika na gari. Wageni walijitambulisha na tuliongeana. Ishaku Bamaiyi pia alichangia dolla 40 kwa UWABA.

Mkutano wa Baisikeli, Nairobi

Mejah, Filbert na Edgar walisafiri Nairobi. Filbert bado anaandika repoti lakini alituelezea kuhusu mkutano. Mkutano ulikuwa na watu wa NGO za baisikeli kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Botswana, Afrika Kusini, Ghana, Burkina Faso, Misri na Uholonzi. Walishiriki kwenye msafara siku ya jumamosi. Kwenye mkutano waliamua kuanzisha Africa Bicycle Network (ABN), na waliandaa malengo ya network. Mkutano uliandaliwa na shirika la Cycling Out of Poverty na Interface for Cycling Expertise. Andrew mwalimu wetu kutoka BEN Afrika Kusini alikuwepo anatusalimia.

Mkutano wa usalama barabarani, Dar es Salaam

Walishiriki kwenye mkutano huu ni: Elaine Baker, Hussein Hamza, Juma Chibaya, Paulo Hatibu, Shukuru Hassan, Ally Athman, Juma S Jongo, Hamadi Bwaja, Shamte Kisoma, Mohammed Samwel, Bashiri Rashid, Sosthenes Amlima, Abduli Mwaibambe, Rahma Ali, Mejah Mbuya, Filbert Mbecha na Edgar Paulo (siku mbili tu), Prosper Nyaki (siku mmoja tu).

Hamadi aliandika repoti na Elaine atachapa.

Mkutano uliandaa malengo madogo ili kufikisha lengo kubwa la kupunguza idadi ya vifo barabarani kwa asilimia 50% kabla ya 2015. Pia mkutano ulitayarisha kwa mkutano wa mawaziri Russia mwisho wa mwaka huu.

Wanachama wa UWABA walipata nafasi ya kutana na watu mbali mbali wa hapa Tanzania na nje ya nchi wanaohusika na usalama barabarani, na pia kuchangia kidogo kwenye mazungumzo. Komanda James Kombe alitualika tutembelee ofisi yake. Pia alisema tutoe repoti kuhusu magari wanaovunja sheria pamoja na picha ofisini kwake.

Picha ya wanachama wa UWABA pamoja na Michelle Yeoh, Mbalazi wa Usalama Barabarani, zilikuwa ndani ya gazeti ya Majira na gazeti ya Mwananchi.

Mradi wa Wamba

Elaine aliandika barua ya shule ya Mtoni Saba Saba na Imelda alipeleka. Tutapata jibu shule itakapofungua. Bado tunafuatalia contacts za shule zingine.

Msafara

Juma Chibaya alitoa photocopy ya proposal. Bashiri, Elaine, Sosthenes, Kibwana, Paulo, Juma na Filbert wote watatafuta wadhamini wiki hii.

Kutafuta mikutano

Elaine ataandika barua za kutafuta mikutano na Meya wa Dar es Salaam, Waziri wa Miundombinu, Madiwani ya Jiji, Komanda James Kombe. Pia tualike watu wa serikali ya mtaa (mwenyekiti wa mtaa, mtendaji wa kata).

Uchaguzi wa 2010

Kwenye mkutano wa Usalama Barabarani tulipewa wazo na Rosa Mang'anya kwamba tujaribu kuhakikisha usalama barabarani uwe ndani ya liani za uchaguzi za vyama mbali mbali. Elaine ataandika barua kwa wenyekiti wa vyama kuwauliza ilani za uchaguzi zinaandikwa lini na vipi sisi tunaweza kuchangia mawazo. Paulo ameshapata ilani ya 2005 ya TLP na Elaine anayo ya CCM. Paulo atatafuta za vyama vingine.

Marekebisho madogo madogo ya barabara

Elaine alipendekeza kila mwanachama anayeona matatizo ya barabara aandike barua kwa mkono na yeye atachapa.

Mafunzo ya Lugha

Hamadi alisema lazima tuendelee na mafunzo ya lugha kwa sababu ni tatizo kuwasiliana na wageni wa nje ya nchi.

Hela na guta

Elaine alilipa Tsh 24,000 kwa wanachama waliohudhuria mkutano wa usalama barabarani (Tsh 2,000 kwa mtu). Pia alilipa Tsh 8,800 kufanya photocopy ya vipeperushi. Pia alilipa Tsh 2,000 kufanya photocopy ya proposal ya msafara. Jumla Tsh 34,800.

Filbert alitumia hela za UWABA kumlipa Tsh 20,000 kwa Juma kwa posho ya mwezi wa sita. Pia alilimrudisha Elaine Tsh 9,000, bado Elaine anadai Tsh 25,800. Sasa Filbert hana hela za UWABA za Tsh. Filbert alipewa kazi kubadilisha dolla 40 ya mchango wa mgeni kwa Tsh.

UWABA tunadai Tsh 22,000 ya hela ya guta.

Mambo mengine

Tutapata reporti ya Tanga Dominata akirudi.

Bado tunasubiri taarifa ya msamaha wa kodi kabla ya kuendelea na mradi wa Re-Cycle.

Kuhusu Fasta courier cooperative – tutakutana na Bwana Bukuku Mejah akiwepo.

Mejah anatayarisha CD cover kwa ajili ya wimbo.

Tutakubali siku ya uchaguzi wa kamati Mejah akiwepo.